# Nyumba za Ibada - Kusawazisha Kusudi na Usalama

Nyumba za Ibada lazima zisawazishe kuwa wazi na kuwakaribisha wote wanaojikinga dhidi ya matukio ya uhalifu. Ni muhimu kwamba usalama ukamilishe misheni inayoegemea imani.

## Mpango

- Bainisha chumba/vyumba katika jengo ambacho/ambavyo kinaweza/vinaweza kutumika kama chumba/vyumba salama iwapo tahadhari ya kutotoka nje au amri ya kutoka ikitolewa.
- Hakikisha kuwa kina mlango mgumu wa chuma wenye kufuli madhubuti.
- Hakikisha kina simu au njia nyingine za mawasiliano.
- Hakikisha chumba kina chakula cha kutosha, maji, seti au vifaa vya huduma ya kwanza ya kiwewe (ikiwemo tourniquet, vitambaa vya kuziba majeraha ) na vilevile choo au choo cha watu wenye ulemavu wa viungo.
- Zingatia kujumuisha vitu vya ziada vinavyoweza kutumika kukinga mlango (yaani kamba au ukanda kwa utaratibu wa kujifunga).
- Anzisha eneo la kukimbilia nje ya kituo iwapo dharura itatokea.
- Wapange watu wa kujitolea na/au mabawabu kimkakati wakati wote wa mkutano (yaani barazani, karibu na njia za kutokea) ili kuangalia na kushughulikia shughuli zinazotiliwa shaka.
- Watumie watu wa kujitolea kusimamia milango kabla, wakati na baada ya huduma.

## Jiandae

- Wape majukumu wafanyikazi wakati wa hali ya zuio la kutoka nje, ikiwemo:
  - Kufunga kwa ufunguo milango ya nje.
  - Kufunga milango ya ndani ili kuongeza vizuizi.
  - Fagia kituo na uwaelekeze watu kwenye chumba cha zuio la kutoka nje.
  - Fikiria kazi maalum za ziada za kituo.
- Tunza kiendeshi cha USB au faili yenye ramani au michoro ya jengo; orodha ya wafanyikazi, washiriki na watu wa kujitolea; masuala maalum ambayo yanaweza kuwepo kwenye kituo (kama vile kituo cha kulelea watoto mchana), n.k. kwa ajili ya utekelezaji wa sheria.
- Mtambue mtu atakayetumika kama mtu wa kuwasiliana naye kwa ajili ya utekelezaji wa sheria.
- Fanya mazoezi ya zuio la kutoka nje na uokoaji wa dharura mara nyingi.
- Zingatia kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na watu wa kujitolea kuhusu mada kama vile usalama wa mtu binafsi na vurugu za mahali pa kazi.

# Mikakati Makini

Mpango wa kina wa usalama huanza na kusudi na nia. Kuteua kikundi cha washiriki wa mkutano kutathmini na kuunda sera na mpango unaozingatia usalama na kushughulikia mgogoro ni jambo la msingi.

- Ratibu pamoja na vyombo vya Utekelezaji wa Sheria/Kuzuia Uhalifu kwa ajili ya Tathmini ya Usalama.
- Hakikisha kwamba masuala ya usalama na ulinzi yanashughulikiwa kwa wakati na kwa njia iliyoratibiwa.
- Shirikiana na vyombo vya Utekelezaji wa Sheria/Kuzuia Uhalifu ili kutoa mafunzo ya ziada kwa wafanyakazi, watu wa kujitolea na washiriki wa mkutano.
- Kuza utamaduni wa kuripoti kuhusu shughuli zinazotiliwa shaka, "ukiangalia kitu, sema kitu."

# Nyenzo za Ziada

https://www.dhs.gov/publication/dhs-faith-based-guidance

ALBUQUERQUE POLICE
ONE ALBUQUERQUE APD